KUSALI INJILI YA LUKA KATIKA FAMILIA ZENU

1. SALA YA KUANZIA:

*- Kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. **W**. Amina*

- SALA YA MTAKATIFU LUKA

EWE! MTUMISHI MPENDWA LUKA.
ULICHAGULIWA KUFUNUA UPENDO WA **M**UNGU
KWA MASKINI KUPITIA MAHUBIRI YAKO.
KWA KUGUSWA NA ROHO WA UPENDO
WA MBINGUNI,
ULIELEZA KWA UWAZI MAISHA YA **Y**ESU,
KWA KUONYESHA UBINADAMU
NA UMUNGU WAKE NA HURUMA YAKE
YA DHATI KWA BINADAMU WOTE.

EWE! **R**OHO **M**TAKATIFU, MWALIMU MWEMA
UNISAIDIE KUELEWA MANENO YAKE **Y**ESU **K**RISTO
NA KUSIKIA HABARI NJEMA YA WOKOVU.
ILI, NIWEZE KUISHI HABARI NJEMA
KWA UAMINIFU KATIKA MAISHA YANGU
AMINA!

2. KUSOMA SURA MOJA YA INJILI:

Katika masomo juu ya ukurasa unaofuata.

3. SALA YA KUFUNGA:

Ee! Mungu, Bwana wetu, tunakushukuru kwa Neno Lako la Uzima katika Injili ya Luka. Tumeshasikia Neno Lako kwa moyo wote; ujaze mioyo, akili na hekima yetu, ili tuishi somo ambalo tumelosoma leo; ujaze pia upendo katika mioyo yetu, ili tulipende Neno Lako zaidi na zaidi. Tunaomba hayo kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu.
AMINA!

INJILI YA LUKA *(Soma sura)*	MWEZI/TAREHE *(Uandikie chini)*	✓
Lk 1		☐
Lk 2		☐
Lk 3		☐
Lk 4;5		☐
Lk 6		☐
Lk 7;8		☐
Lk 9		☐
Lk 10;11		☐
Lk 12		☐
Lk 13;14		☐
Lk 15		☐
Lk 16		☐
Lk 17		☐
Lk 18		☐
Lk 19		☐
Lk 20		☐
Lk 21		☐
Lk 22		☐
Lk 23		☐
Lk 24		☐

SHIRIKA LA NENO LA MUNGU

SVD

e mail: kensvdbpm@gmail.com

© 2019 - Bible Ministry Kenya/Tanzania Province

WOULD YOU LIKE TO BECOME MISSIONARY IN THE DIVINE WORD MISSIONARIES ?

VOCATION DIRECTOR'S OFFICE
Fr. Geoffrey kamau, SVD,
kamaugeoffrey@hotmail.com,
+254701689336

IJUE LUKA INJILI YA

SHIRIKA LA NENO LA MUNGU

© 2019 - Bible Ministry Kenya/Tanzania Province

IJUE SHUGULI ZA UTUME WETU KATIKA KANISA KATOLIKI NA INJILI YA LUKA

Kwa sababu, Papa Benedikto XV katika Waraka wake Kitume "*Maximum Illud—1919*", yaani "Kuhusu Shughuli za Kimisionari" alifungua rasmi ukurasa mpya wa maisha na utume wa Kanisa mintarafu shuguli za kimisionari, kwa kulitaka Kanisa kuanzisha mchakato wa majiundo na malezi kwa ajili ya kuyategemeza Makanisa mahalia kwa rasilimali watu, yaani wahudumu wa Injili.

Baba Mtakatifu Francisko anasema, kwamba utume wetu katika Kanisa Katoliki linapaswa kujiekeleza zaidi katika utekelezaji wa shughuli kama: kuwaongoza Wakristo wote kukutana na Kristo Yesu kwa njia ya Ekaristi Takatifu, Neno la Mungu na Sala.

Mtakatifu Luka anaweza kuitwa kihalali Mwinjili wa utume. Ijapokuwa waandishi wote wa Injili wanathibitisha utume wa Kristo na Kanisa, Luka hutoa maelezo mengi katika Injili yake. Kwa mfano Luka anabainisha kuwa katika huduma ya Yesu ya hadharani anachagua wafuasi 72 na kuwatuma kwenye utume. Maana hayo utume huu wa Ufalme wa Mungu na Kanisa ni kwajili ya Wakristo wote waliobatizwa, si wanafunzi 12 wa Yesu tu, ama Masista, Mabruda na Mapadre pekee.

Kwa hiyo, Utume si mradi wa mtu moja ama binafsi, lakini ni juhudi ya Wakristo wote. Kila aliyebatizwa ameitwa na Mungu kujitolea katika Utume wa Kanisa, kuwa shahidi wa uaminifu wa habari njema, katika maisha yake, familia yake, jumuiya yake hadi pembe zote za ulimwengu.

IJUE INJILI YA LUKA

1 MWINJILI LUKA NI NANI

Katika Kanisa Katoliki Mtakatifu Luka au Mwinjili Luka anajulikana kama Mwandishi wa Injili na kitabu cha Matendo ya Mitume. Mt. Luka (mwinjili) alizaliwa huko Antiokia, iliokuwa iko mkoa wa Syria wakati wa kipindi cha Dola ya Kirumi. Kanisa Katoliki linasherehekea sikukuu yake tarehe 18 Oktoba. Alikuwa mmojawapo wa wainjilishaji wanne. Mwinjili Luka anayefikiriwa na Kanisa Katoliki, kama mlinzi wa wasanii, waganga, madaktari wa upasuaji, wanafunzi na wachinjaji, kwa sababu alikuwa daktari, mchoraji na mwalimu wa tamaduni mbalimbali.
Alibatizwa na Mtakatifu Paulo, kwa hiyo, alikuwa mtoto wake wa kiroho na kila wakati alisafiri na Mtume Paulo.

2 NANI ALIIANDIKA INJILI YA LUKA

Kuhusu mwandishi wa Injili tunategemea tu mapokeo ya zamani kwani hakuna mwandishi aliyesaini jina lake katika Injili hii wala nyingine yoyote. Mapokeo hayo, yanamtaja Luka kuwa mwandishi wa Injili ya tatu. Luka huyo anatajwa kuwa ni daktari wa mji wa Antiokia *(Wakolosai 4:14)*, na pia alikuwa rafiki wa mtume Paulo *(2Timotheo 4:11; Filemoni 24)*, na mwenzi wa Paulo katika safari zake za kimisionari *(Matendo ya Mitume 16:10-18; 20:5-15; 21:1-18; 27:1-28:16)*.

3 INJILI YA LUKA ILIANDIKWA LINI NA WAPI

Kwa hakika, Injili hii iliandikwa baada ya anguko la Yerusalemu katika mwaka 70 BK., maelezo ya anguko hili yanayotolewa katika - *Lk 21:5-38* . Yaani, Injili ya Luka inafahamu kubomolewa kwa Yerusalemu na Warumi mwaka wa 70 BK. *(Lk 13:35; Lk 19:43-44; Lk 23:28 -31)*. Mtazamo mzima wa Injili unaonesha wahusika wake, kama kizazi cha pili au cha tatu cha wakristo. Kwa ujumla, baada ya kuandikwa Injili ya Marko na Mathayo. Kwa hiyo, Injili ya Luka yakadiriwa kuandikwa kati ya mwaka 80 BK hadi 85 BK.
Mahali ilipoandikwa, Je? kutokana na mtazamo mpana wa kimataifa katika Injili na lugha sanifu ya kigiriki iliyotumika, kwa ujumla, tunaweza kusema mahali fulani katika eneo la Ugiriki panaweza kuwa ndipo ilipoandikwa Injili.

4 INJILI YA LUKA ILIYEANDIKWA KWA NANI

Injili inaanza kusema iliyeandikwa kwa Theofilo - *(Lk 1:1-3)*. "Theofilo" maana yake mpendwa wa Mungu. Jina hili laweza kumaanisha mtu binafsi anayeitwa hivyo, vilevile laweza kumaanisha mtu au mwamini yeyote aliyependwa na Mungu, na tafsiri hiyo ya mwisho inaugwa mkono na wengi zaidi leo. Juu ya hayo, wataalamu wa maandiko matakatifu husema kwamba kusoma Injili ya Luka inaweza kupata wapokeaji wa kweli wa Injili. Kwa hiyo, wataalamu husema kwamba Injili hii iliandikwa kwa watu wa mataifa, zaidi wakiwa wagiriki, au walie ambao huongea lugha ya kikirigi. Pamoja na hayo, Jumuiya ndogo ndogo za kikristo zilienea katika Dola ya kirumi, hata Jumuiya za kitamaduni za Paulo. Mfano, Jumuiya zote ambazo zinaweza kutambuliwa zinazofuata:
Jumuiya za ***Miji*** *(Lk 2:1; Lk 3:1-2; Lk 7:11-13; Lk 10:13-15; Lk 19:1-2)*,tofauti kabisa katika jumuiya za *vijiji* za wapalestine.
Jumuiya zinazojumuishwa kama ***Masikini*** or ***Wahitaji*** *(Lk 1:52-53; Lk 4:18; Lk 6:20-23; Lk 7:22)*, ***Matajiri*** *(Lk 6:24-26; Lk 12:16-21; Lk 16:19-31)*, ***Wanawake*** *(Lk 1:26-55; Lk 2:41-52; Lk7:36-48; Lk 8:1-3; Lk 10:38-42; Lk 13:10-13, K.D.)*, na ***Umati wa watu*** or ***Makundi ya watu*** *(Lk 6:17-19; Lk 7:24; 8:4.40; 12:54; Lk 9:11-16.18-21.37; Lk 13:17)*.

5 INJILI YA LUKA INA MAMBO GANI AMBAYO HAYAPATIKANI KATIKA INJILI ZINGINE

Injili ya Luka yenyewe ni ya kipekee zaidi kuliko Injili yeyote katika Agano Jipya. Kwa mfano, tuangalie kila kipengele ambacho kionekana tu katika Injili yake, kama inavyofuata:
Masimulizi yote ya Sura ya kwanza (Lk 1:5-80)
Yesu anatolewa Hekaluni (Lk 2:22-24)
Utume wa sabini na wawili (Lk 10:1-12)
Msamaria mwema (Lk 10:25-37)
Simulizi la Mwanapotevu (Lk 15:11-32)
Simulizi la Farisayo na Mtoza ushuru (Lk 18:9-13)
Simulizi la Zakayo Mtoza ushuru mkuu (Lk 19:1-10)
Safari ya Emau (Lk 24:13-35)

Maandiko hayo ya Biblia yanapatikana tu katika Injili ya Luka pekee.



Yaani 35% ya yaliyomo pekee yanatoka Injili yenyewe na yaliyomo nyingine 65% yanaweza kupatikana katika Injili zingine mbili, Marko na Mathayo. Yaliyomo kwenye Injili tatu: Marko, Mathayo na Luka huitwa Injili za Sinoptics, ambayo inamaanisha mtazamo sawasawa.

6 MBONA NG' OMBE NI ISHARA YA INJILI YA LUKA

Injili ya Luka inaanza kusimulia hadithi ya Zakaria, ambaye alikuwa kuhani katika hekalu la Yerusalemu; Huduma yake ilikuwa kufukiza ubani na kuchinja wanyama waliopewa kama sadaka - hasa kafara ya ng'ombe - *(LK 1:5-8)*; Ndiyo maana ishara ya Injili ya Luka ni Ng'ombe anayeashiria sadaka. Mbona Ng'ombe anashiria sadaka? kwa sababu ng'ombe alikuwa mnyama anayethaminiwa zaidi kwa sadaka ya tamaduni ya Kiyahudi na hasa katika nyakati za Yesu. Sababu nyingine ni kwamba, Luka anamchukua Yesu kama sadaka halisi kwa ulimwengu wote, yaani, Yesu ndiye Mwokozi wa ulimwengu na Njia ya wokovu kwa wote.

7 MBONA INJILI YA LUKA INAITWA INJILI YA NJIA AMA INJILI YA HURUMA

Kitu cha muhimu sana katika Injili ya Luka ni matembezi ambayo Yesu hufanya kutoka Galilaya kwenda Yerusalemu. Ndiyo matembezi ya kuvutia yanayoaanza huko Galilaya, yanaendelea hatua kwa hatua, kwenye barabara hii ya kwenda Yerusalemu hadi pale penye mji mkuu wa Yerusalemu *(Lk 9:51-19:27)*; na vilevile safari ya kwenda Emau *(Lk 24:13-35)*. Kwa hiyo, takribani nusu ya Injili inazungumza kuhusu Yesu akitembea njiani, kutoka Galilaya kwenda Yerusalemu, na pia akitembea Emau - Ndiyo sababu, Injili ya Luka inaitwa *"Injili ya Njia"* na Wataalamu wengi wa Biblia.
Vile vile Wataalamu wa Biblia husema kwamba Injili ya Luka inaweza kuitwa Injili ya Huruma. Kwa sababu vifungu vingi vya Injili vinaangazia rehema, ubadilifu na huruma. Ndiyo sababu, kwamba sura 15 nzima ni moyo na ufunguo wa Injili hii. Tena, sababu nyingine inawezekana katika Injili ya Luka pekee, ni simulizi la mwanampotevu *(Lk 15: 11-32)* na msamaria mwema, *(Lk 10:15-37)*, kuhusu mada ya Huruma.

8 KATIKA INJILI YA LUKA, YESU WA NAZARETI NI NANI NA KUMFUATA MAANA YAKE NI NINI

Yesu ndiye "Mwokozi wa ulimwengu" *(Lk 2: 30-32; Lk 24; 47)*, "Mkombozi wa masikini, waliokandamizwa na waliotengwa "*(Lk 4: 18-19; Lk 6:17-26)*," Bwana "*(Lk 1:43; Lk 5: 8)*, "Kufunua huruma ya Baba" (Lk 15: 1-32), "Nabii wa Mungu" *(Lk 24:19)*,
Mmoja wa matendo mengi na sala nyingi *(Lk 6:12; Lk 11:1-13)*.
Kuwa mwanafunzi ni kutembea na Yesu wa Nazareti *(Lk 9:57-62)*, kuwa mwenye huruma *(Lk 10:29-37)*, jihadharini na aina yoyote ya uchoyo na moyo mgumu *(Lk 12:33-34)*, kuwa mtumishi wa Bwana *(Lk 12:35-49)*, mwishoni , kufanya kama Yesu alivyosema, mfuate *(Lk 14: 25-33)*.